JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# WIZARA YA KILIMO
# BODI YA KOROSHO TANZANIA



# JARIDA LA MWEZI
## Februari 2024.

Toleo Jipya

#KilimoBiashara

## 1.0 UTANGULIZI

Msimu wa Korosho nchini Tanzania huanza mwezi Oktoba na kuisha mwezi wa Aprili, hii ni baada ya Mikoa mipya kuanza kuzalisha korosho. Hata hivyo zaidi ya asilimia 90 ya korosho ghafi huzalishwa katika mikoa ya kusini mwa Tanzania ambayo ni Mtwara, Lindi, Ruvuma na Pwani ambayo msimu wake ni kuanzia Oktoba hadi Mwezi Januari. Mpaka sasa minada katika mikoa hiyo tayari imesitishwa. Kiasi kidogo cha korosho zilizobaki kwa wakulima zinaendelea kuuzwa kwa wabanguaji wa ndani kupitia Soko la awali. Kwa upande wa kanda ya Kaskazini na kanda ya kati, hususani mikoa ya Tanga, Dodoma na Singida mavuno huanza mwezi wa Februari hadi Aprili lakini kutokana na kukithiri kwa mvua mavuno ya korosho kwa kanda hii yamechelewa kuanza, hivyo mpaka sasa hakuna mkoa wa kanda hizo ulioanza kufanya minada kama ilivyozoeleka kwa misimu mingine.



## 2.0. MWENENDO WA SOKO LA KOROSHO KATIKA NCHI MBALIMBALI DUNIANI MWEZI FEBRUARI, 2024.

### 2.1. MWENENDO WA SOKO AFRIKA MAGHARIBI

Nchini Ivory Coast ufunguzi rasmi wa msimu umefanyika tarehe 21 Februari, 2024 baada ya mkutano wa baraza la Rais uliofanyika tarehe 20, Februari, 2024. Bei rasmi iliyopitishwa kisheria kwa korosho ghafi zilizokaushwa vizuri zimepangwa kama ifuatavyo:

**Jedwali Na. 1: Bei Elekezi Nchini Ivory Coast kwa msimu wa 2024**

| Na | Aina | Kiasi (Tsh/Kg) |
|---|---|---|
| 1 | Bei katika Ngazi ya Mkulima | 1,168.75 |
| 2 | Ghala la Msingi ( Maeneo ya kununulia) | 1,275.00 |
| 3 | Ghala la kiwanda | 1,398.00 |
| 4 | Ghala la wasafirishaji (Maeneo ya Kununulia) | 1,462.00 |
| 5 | Bandari kavu ya Bouake' | 1,462.00 |
| 6 | Ghala la Abidjan | 1,525.75 |

**Chanzo:** Cashewnutinformation

Wabanguaji wengi wanahisi kwamba bei katika ngazi ya mkulima imebaki kuwa kubwa ukilinganisha na bei ya korosho karanga iliyopo kwa sasa, kwa upande mwingine wazalishaji wa korosho ghafi wanatarajia kupanda kwa bei. Masafirisho ya korosho kwenda nje ya nchi yanatarajia kuanza wiki ya tatu ya mwezi Machi.

**Chanzo:** African Cashew Alliance

Kwa upande wa nchi ya Ghana msimu mpya tayari umeanza na bei ya korosho imepungua baada ya kutangazwa kwa bei rasmi nchini Ivory Coast. Wanunuzi wengi wamepunguza bei kati ya Dola za Kimarekani 0.78 na 0.85 (Shilingi 1,983 na 2,161) kwa kilogramu kwa korosho zinazopokelewa kwenye Ghala la wasafirishaji. Bei ya korosho zikiwa zimefika Bandari ya Tema ni kati ya Dola za Kimarekani 0.95 hadi 0.97 (Shilingi 2,415 hadi 2,466) kwa kilo.

**Chanzo:** African Cashew Alliance

Nchini Nigeria tayari msimu wa mauzo umeanza na bei ya korosho ghafi ipo juu na uuzwaji wa korosho ni wa taratibu mno. Bei ya korosho ghafi ni kati ya Dola za Kimarekani 0.739 hadi 0.873 (Shilingi 1,879 hadi 2,220) kwa kilo kwa korosho zenye ubora wa ratili 48 hadi 52 huku kiwango cha unyevu ni kati ya 10% hadi 11%. Shughuli za masafirisho ya korosho ni ya kiwango cha chini hii ni kutokana na kupanda kwa kasi kwa kiwango cha ubadilishaji cha Naira dhidi ya Dola ya kimarekani.

**Chanzo:** African Cashew Alliance

Kwa upande wa Guinea Bissau msimu wa mauzo ya korosho umeanza na bei rasmi iliyotangazwa katika ngazi ya mkulima ni Dola za Kimarekani 0.50 (shilingi 1,271) kwa kilo.Nchini Gambia na Senegal hali ya kiwango cha joto kuwa chini ukilinganisha na miaka michache iliyopita, mazao yanaonekana kuchelewa kuwa tayari kama nchi jirani. Kampeni za masoko ya korosho nchini Senegal zitaanza tarehe 15 March, 2024.

**Chanzo:** African Cashew Alliance

**2.2. Hali ya Soko la Korosho Nchini India**

Nchini India masoko ya ndani ya korosho ghafi yamechelewa kuanza kwa wiki chache kitendo kinachoashiria uwezekano wa kuwepo kwa mavuno machache kwa msimu huu, hata hivyo, India inaagiza karibu asilimia 65 ya korosho kutoka nchi za Afrika. Bei ya korosho inayoagizwa kutoka nchi za Afrika kwa mwezi Februari ni kati ya Dola za Kimarekani 1,010 hadi 1,150 kwa tani (CIF) kwa ubora wa Ratili 49 hadi 51 (48-51lbs).

Mahitaji ya ndani ya korosho karanga yanaonekana kutoongezeka kama ilivyotarajiwa. Hakuna mabadiliko ya bei katika miezi michache iliyopita hasa baada ya tamasha la Diwali.

**Chanzo:** Cashewnutinformation

**2.3. Hali ya Soko la Korosho katika Nchi ya Vietnam**Nchini India Nchini Vietnam soko la korosho ghafi bado limeendelea kuwa thabiti, ingawa bado kuna mahitaji ya korosho ghafi kutoka Afrika, ila bei imeendelea kuwa kubwa ukilinganisha na bei ya korosho karanga. Wabanguaji wakubwa hawajanunua kiasi chochote cha korosho ghafi kwa msimu huu, bado wanaendelea kusubiri waki-amini bei ya korosho ghafi inapaswa kushuka zaidi au bei ya koro-sho karanga inapaswa kupanda zaidi. Bei ya korosho ghafi kutoka Afrika ni kati ya Dola za kimarekani 1,040 (CIF) kwa tani hadi 1,110 (CIF) kwa tani kwa ubora wa Ratili kati ya 49 (lbs) hadi 50 (lbs). Mauzo ya nje ya korosho karanga katika nusu ya kwanza Februari 2024 ni tani 11,836 zenye thamani ya Dola za Kimarekani 64,200,000 (wastani wa bei ya Dola za Kimarekani 5,424 kwa tani).


**Chanzo:** Cashewnutinformation



## Jedwali Na 2:Bei za Korosho Ghafi Katika Nchi ya India na Vietnam Februari, 2024

| MWENENDO WA BEI ZA WASTANI ZA KOROSHO GHAFI DUNIANI INDIA NA VIETNAM KWA KIPINDI CHA JANUARI 2023 HADI FEBRUARI 2024 | | |
|---|---|---|
| TARAHE | Bei - CIF USD / TON | |
| | BEI YA CHINI | BEI YA JUU |
| 28 Januari, 2023 | 1,250 | 1,390 |
| 18 Februari, 2023 | 1,180 | 1,230 |
| 13 Machi, 2023 | 1,150 | 1,165 |
| 24 April, 2023 | 1,040 | 1,080 |
| 20 Mei, 2023 | 1,040 | 1,130 |
| 18 Juni, 2023 | 925 | 1,065 |
| 22 Julai, 2023 | 925 | 1,080 |
| 21 Agosti, 2023 | 950 | 1,080 |
| 23 Septemba, 2023 | 1,030 | 1,165 |
| 16 Octoba, 2023 | 1,030 | 1,165 |
| 25 November, 2023 | 1,180 | 1,230 |
| 26 Desemba, 2023 | 1,080 | 1,190 |
| 14 Januari, 2024 | 1,060 | 1,100 |
| 24 Februari, 2024 | 1,040 | 1,150 |
| SOT: 48-53 | | |

**Chanzo:** Cashewnutinformatio




**Chanzo:** Cashewnutinformatio

## 3.0 BEI ZA KOROSHO KARANGA KUTOKA NCHI MBALIMBALI DUNI

Bei ya korosho karanga katika nchi mbalimbali hutofautiana kwa kuzingatia kiwango cha uzalishaji, gharama za uzalishaji, viwango vya ubora pamoja na teknolojia inayotumika kubangua korosho ghafi.

### 3.1 Bei ya Korosho Karanga Vietnam Kufikia FEBRUARI, 2024

Nchini Vietnam bei ya korosho karanga iko chini kidogo ikilinganishwa na bei katika nchi zingine zinazobangua korosho. Kuna mabadiliko ya bei kwa mwezi Februari kama inavyoonekana kwenye Jedwali Na. 3

**Jedwali Na. 3: Bei za Korosho Karanga Nchini Vietnam hadi kufikia Novemba, 2023**

| BEI YA KOROSHO KARANGA VIETNAM HADI KUFIKIA Novemba, 2023 | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| MAUZO YA DARAJA | DARAJA | Bei Dola/Kilo (FOB) | | Bei TZS/Kilo (FOB) | |
| | | Bei ya Chini | Bei ya Juu | Bei ya Juu | Bei ya Juu |
| White Whole Cashews 180 | 180 WW | 7.61 | 8.38 | 19,344.62 | 21,301.96 |
| White Whole Cashews 210 | WW 210 | 6.50 | 7.06 | 16,523.00 | 17,946.52 |
| White Whole Cashews 240 | WW240 | 5.78 | 6.06 | 14,692.76 | 15,404.52 |
| White Whole Cashews 320 | WW320 | 5.07 | 5.40 | 12,887.94 | 13,726.80 |
| Large Pieces | LP | 2.43 | 2.65 | 6,177.06 | 6,736.30 |
| Small Pieces | SP | 1.76 | 1.98 | 4,473.92 | 5,033.16 |

**Chanzo:** Cashewinformation

### 3.2 Bei ya Korosho Karanga katika nchi za Afrika Magharibi Hadi Kufikia Februari, 2024

Hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Februari, bei ya korosho karanga kwa nchi za Afrika Magharibi ambazo ni Ivory Coast, Ghana, Benin nk. Inakadiriwa kuwa kama inavyoonekana kwenye Jedwali Na. 4

**Jedwali Na. 4: Bei ya Korosho Karanga Afrika Magharibi hadi Kufikia Februari, 2024**

| BEI YA KOROSHO KARANGA AFRIKA MAGHARIBI HADI KUFIKIA FEBRUARI, 2024 | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| MAELEZO YA DARAJA | DARAJA | Bei Dola/Kilo (FOB) | | Bei TZS/Kilo (FOB) | |
| | | Bei ya Chini | Bei ya Juu | Bei ya Chini | Bei ya Juu |
| White Whole Cashews 180 | W180 | | | | |
| White Whole Cashews 180 | W210 | 7.06 | 7.17 | 17,946.52 | 18,226.14 |
| White Whole Cashews 240 | W240 | 5.84 | 6.06 | 14,845.28 | 15,404.52 |
| White Whole Cashews 320 | W320 | 5.29 | 5.62 | 13,447.18 | 14,286.04 |
| White Whole Cashews 450 | W450 | 5.07 | 5.29 | 12,887.94 | 13,447.00 |
| White Splits | WS | 3.31 | 3.53 | 8,414.02 | 8,973.26 |
| Large Pieces | LP | 2.65 | 3.09 | 6,736.30 | 7,854.78 |
| Small Pieces | SP | 2.21 | 2.43 | 5,617.82 | 6,177.06 |

**Chanzo:** Tanzania Association for Cashewnut Processors **(TACP)**

### 3.3 Bei ya Korosho Karanga Tanzania Zinazouzwa Nje ya Nchi Hadi Kufikia Februari, 2024


Bei ya korosho karanga zinazobanguliwa na wabanguaji wa ndani na kuuzwa nje katika nchi za Uholanzi, Uturuki, Misri, nchi za Uarabuni, Marekani nk. Kuna mabadiliko kidogo ya bei kama inavyoonekana katika jedwali Na. 5

**Jedwali Na. 5: Bei ya Korosho Karanga Tanzania Zinazouzwa Nje ya Nchi hadi kufikia Februari, 2024.**

| BEI YA KOROSHO KARANGA TANZANIA ZINAZOUZWA NJE HADI KUFIKIA FEBRUARI, 2024 | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| MAELEZO YA DARAJA | DARAJA | BEI DOLA/KILO (FOB) | | BEI TZS/KILO (FOB) | |
| | | Bei ya Chini | Bei ya Juu | Bei ya Chini | Bei ya Juu |
| WHITE WHOLE CASHEWS 180 | W180 | 7.80 | 8.15 | 19,500.00 | 20,375.00 |
| WHITE WHOLE CASHEWS 240 | W240 | 6.70 | 7.20 | 16,750.00 | 18,000.00 |
| WHITE WHOLE CASHEWS 320 | W320 | 6.05 | 6.80 | 15,125.00 | 17,000.00 |
| WHITE SPLITS | WS | 4.60 | 4.80 | 15,500.00 | 12,000.00 |
| LARGE WHITE PIECES | WS | 4.10 | 4.30 | 10,250.50 | 10,750.00 |

**Chanzo:** Tanzania Association for Cashewnut Processors **(TACP)**

**JEDWALI NAMBA 6: UWIANO WA BEI DARAJA WW320**




**Chanzo:** Bodi ya Korosho

## 4.0 MWENENDO WA ZAO LA KOROSHO NCHINI TANZANIA

Hadi kufikia tarehe 29 Februari, 2024 uzalishaji wa korosho ghafi kwa msimu wa 2023/2024 ni tani 254,212.981 zenye thamani ya shilingi 468,660,044,484.00 ambapo tani 244,646.026 zimekusanywa na kuuzwa katika ghala za minada zenye thamani ya shilingi 454,016,863,103.00. Mauzo ya korosho kupitia soko la awali hadi kufikia wiki ya mwisho ya mwezi Februari ni tani 5,492.875 zenye thamani ya shilingi 8,532,062,131.00 na korosho zilizobanguliwa na wabanguaji wadogo ni takribani tani 905.351 sawa na tani 4,074.080 za korosho ghafi zenye makadirio ya thamani ya shilingi 6,111,119,250.00. Ukusanyaji wa takwimu za uzalishaji unaendelea.

Shughuli ya utoaji wa vibali vya kusafirisha Korosho ghafi nje ya nchi inaendelea ambapo hadi kufikia tarehe 29 Februari, 2024 zaidi ya tani 239,975.492 za korosho ghafi zenye thamani ya Dola za Kimarekani 227,229,537.26 (FOB Value) zimepatiwa vibali vya kusafirisha nje ya nchi. Pia vibali vya kusafirisha korosho karanga vinaendelea kutolewa na hadi sasa zaidi ya tani 1,462.965 zenye thamani ya Dola za Kimarekani 7,337,624.26 (FOB Value) zimesafirishwa.

Hadi kufikia tarehe 29 Februari, 2024 jumla ya tani 219,087.94 sawa na asilimia 97.6 (97.6%) ya korosho zote zilizosafirishwa kwenda nchi za nje zimesafirishwa kupitia bandari ya Mtwara na tani 5,373.35 sawa na asilimia 2.39 (2.39%) za korosho zote zilizosafirishwa kwenda nje ya nchi zimesafirishwa kupitia Bandari ya Dar es Salaam na kufanya jumla ya tani 224,461.29 zimesafirishwa kwenda nje ya nchi ambazo ni sawa na asilimia 91.73 (91.75%) ya mauzo ya korosho zote kupitia mfumo wa stakabadhi za ghala ambazo ni tani 244,646.026.



## JEDWALI NA. 7a: TAARIFA YA UZALISHAJI KOROSHO MSIMU WA 2023/2024 HADI KUFIKIA MWEZI FEBRUARI, TAARIFA YA UZALISHAJI KOROSHO MSIMU WA 2022/2023 HADI KUFIKIA TAREHE 29/02/2024

| | MKOA | CHAMA KIKUU | GHALA ZA MNADA (KG) | THAMANI GHALA ZA MNADA (TSHS) | SOKO LA AWALI (KG) | THAMANI SOKO LA AWALI (TSHS) | ZILIZO BANGULIWA (KG) | | THAMANI UWIANO WA GHAFI (TSHS) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | ZILIZO BANGULIWA | UWIANO WA GHAFI | |
| 1 | MTWARA | TANECU | 74,139,120.00 | 138,419,162,921.00 | 830,962.00 | 1,309,898,850.00 | 771,493.00 | 3,471,718.50 | 5,207,577,750.00 |
| | | MAMCU | 64,994,995.30 | 122,821,597,840.00 | 1,966,705.80 | 3,147,340,130.00 | 86,963.00 | 391,333.50 | 587,000,250.00 |
| 2 | LINDI | RUNALI | 53,508,655.00 | 101,073,643,448.00 | 15,000.00 | 23,250,000.00 | | | |
| | | MWAMBAO | 15,137,180.00 | 27,080,718,970.00 | | | 5,000.00 | 22,500.00 | 33,750,000.00 |
| 3 | RUVUMA | TAMCU | 26,062,323.00 | 45,567,818,324.00 | 110,000.00 | 190,300,000.0 | | | |
| 4 | PWANI | CORECU | 10,614,233.00 | 18,754,736,800.00 | 2,521,687.00 | 3,801,458,151.00 | 41,895.00 | 188,527.50 | 282,791,250.0 |
| 5 | TANGA | TACACU | | | | | | | |
| 6 | SINGIDA | CEAMCU | | | | | | | |
| 7 | MOROGORO | UKICU | 189,520.00 | 299,184,800.00 | 48,520.00 | 59,815,000.00 | - | - | - |
| 8 | TABORA | | | | | | | | |
| 9 | DODOMA | DOMASIKA | | | | | | | |
| 10 | MBEYA | | | | | | | | |
| 11 | NJOMBE | | | | | | | | |
| 12 | KIGOMA | | | | | | | | |
| | JUMLA NDOGO | | 244,646,026.30 | 454,016,863,103.00 | 5,492,874.80 | 8,532,062,131.00 | 905,351.00 | 4,074,079.50 | 6,111,119,250.00 |
| | JUMLA KUU UZALISHAHI | | | | | | | | 254,212,980.60 |
| JUMLA KUU DHAMANI | | | | | | | | | 468,660,044,484.00 |

**NB:** : Taarifa hii ya uzalishaji ni hadi kufikia tarehe 29 Februari, 2024.
Ukusanyaji wa taarifa za uzalishaji bado unaendelea

## JEDWALI NA. 7B: KOROSHO ZILIZOUZWA KUPITIA MFUMO WA STAKABADHI GHALANI.

| Jumla ya Kiasi Kilichouzwa na Thamani (Novemba 21 hadi Novemba 30, 2023) | | |
|---|---|---|
| **KIPINDI CHA** | **KIASI KILICHOUZWA (MT)** | **THAMANI (TZS)** |
| Mwezi wa FEBRUARI | NA | NA |
| Jumlishi Oktoba - Januari | 244,646,026 | 454,016,863,103 |
| **JUMLA** | **244,646,026** | **454,016,863,103** |

## JEDWALI NA. 7C: MUHTASARI BEI ZA KOROSHO GHAFI KATIKA MINADA

| MUHTASARI BEI ZA KOROSHO GHAFI KATIKA MNADA | | | |
|---|---|---|---|
| **MWEZI ILIYOPITA (Januari,2024)** | | **MWEZI YA SASA (Februari, 2024)** | |
| **MWENENDO WA BEI** | **Mwezi** | **Daraja la Kawaida** | |
| | | **Bei ya Juu** | **Bei ya Chini** |
| | Bei ya Mwezi Februari | NA | NA |
| | Bei ya Mwezi Januari | 1,650 | 1,570 |
| | Mabadiliko (%) | | |

**UFUNGUO** "NA"= Haipo

| BEI YA MAUZO KOROSHO GHAFI YA MKOA (JULAI, 2023) | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **MKOA** | **CHAMA KIKUU** | **MWEZI** | **DARAJA LA KAWAIDA** | |
| | | | BEI YA JUU | BEI YA CHINI |
| **MTWARA** | **MAMCU** | Bei ya Mwezi Februari | NA | NA |
| | | Bei ya Mwezi Januari | 1,300 | 1,250 |
| | | **Mabadiliko (%)** | | |
| | **MAMCU** | Bei ya Mwezi Februari | NA | NA |
| | | Bei ya Mwezi Januari | 1,510 | 1,500 |
| | | **Mabadiliko (%)** | | |
| **LINDI** | **RUNALI** | Bei ya Mwezi Februari | NA | NA |
| | | Bei ya Mwezi Januari | 1,650 | 1,550 |
| | | **Mabadiliko (%)** | | |
| | **LINDI MWAMBAO** | Bei ya Mwezi Februari | NA | NA |
| | | Bei ya Mwezi januari | 1,560 | 1,500 |
| | | **Mabadiliko (%)** | | |
| **PWANI** | **CORECU** | Bei ya Mwezi Februari | NA | NA |
| | | Bei ya Mwezi Januari | 1,560 | 780 |
| | | **Mabadiliko (%)** | | |
| **RUVUMA** | **TAMCU** | Bei ya Mwezi Februari | NA | NA |
| | | Bei ya Mwezi Januari | 1,350 | 1,345 |
| | | **Mabadiliko (%)** | | |
| **MOROGORO** | **MOFACU** | Bei ya Mwezi Februari | NA | NA |
| | | Bei ya Mwezi Januari | 1,570 | 1,570 |
| | | **Mabadiliko (%)** | | |

**Ufunguo**: NA= Haipo
Chanzo: Bodi ya Korosho Tanzania

**Chanzo:** Bodi ya Korosho Tanzania

## 5.0 HALI YA UBORA WA KOROSHO MSIMU WA 2023/2024


Hali ya ubora kwa miaka 3 mfululizo imeendelea kuimarika kwa mujibu wa takwimu za mauzo ya korosho hadi kufikia tarehe 29/02/2024. Korosho daraja kwanza zilizoingia mnadani ni tani 240,852.707 ambazo ni sawa na asilimia 98.449 (98.449%) ya korosho zote zilizouzwa kwa njia ya mnada na korosho daraja la pili ni tani 3,793.319 ambazo ni sawa na asilimia 1.551 (1.551%) ya korosho zote zilizouzwa mnadani.

Aidha kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa na mvua nyingi baadhi ya maeneo kumekuwa na changamoto ya kiwango cha unyevu wa korosho na mkoa wa Pwani baadhi ya maeneo korosho zimekosa sifa za kuingia sokoni kwa sababu ya unyevu mkubwa uliosababisha korosho kuota/kuharibika.

Hatua mbalimbali zimeendelea kuchukuliwa katika kusimamia ubora wa korosho ikiwemo kutoa elimu kupitia redio za kijamii na semina kwa wakulima,viongozi wa AMCOS na maafisa kilimo kata/vijiji, kufanya ukaguzi wa mara kwa mara katika ghala za Vyama vya Msingi na ghala za mnada na kununua na kusambaza maturubai ya kuanikia korosho katika Vyama vya Msingi kwaajili ya kuanikia korosho.

## 6.0 ZOEZI LA UHUISHAJI WA KANZIDATA YA WAKULIMA WA ZAO LA KOROSHO

Bodi ya korosho kwa kushirikiana na Halmashauri zinazolima zao la korosho inaendelea na zoezi la kuhuisha kanzi data ya wakulima wa korosho. Hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Februari tayari mikoa ya Mtwara, Lindi na Ruvuma imehuisha kanzi data za wakulima. Zoezi bado linaendelea ambapo mpaka sasa jumla ya wakulima 263,597 sawa na asilimia 47 ya wakulima waliosajiliwa wamefikiwa na kuhuishwa taarifa zao ikiwa ni Pamoja na kutambua ukubwa wa mashamba yao (kuchukua coordinates), idadi ya mikorosho, picha za wakulima na taarifa zingine za muhimu katika Halmashauri za mikoa ya Mtwara, Lindi na Ruvuma kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 8. Aidha, Usajili wa Wakulima bado unaendelea.



**Jedwali Na. 8 Taarifa ya Mwenendo wa Uhuishaji wa Kanzidata ya Wakulima wa zao la Korosho.**

| Na | Mkoa | Halmashauri | Idadi ya Wakulima Waliofikiwa |
|---|---|---|---|
| 1 | Mtwara | Manispaa ya Mtwara | 1,937 |
| | | Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara | 15,790 |
| | | Halmashauri ya Wilaya ya Nanyamba | 26,593 |
| | | Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba | 66,872 |
| | | Halmashauri ya Wilaya ya Newala | 10,536 |
| | | Halmashauri ya Mji Newala | 5,378 |
| | | Halmashauri ya Wilaya ya Masasi | 37,851 |
| | | Halmashauri ya Mji Masasi | 6,343 |
| | | Halmashauri ya Wilaya ya Nanyumbu | 18,747 |
| 2 | Lindi | Manispaa ya Lindi | 3,092 |
| | | Halmashauri ya Mji Mtama | 18,790 |
| | | Halmashauri ya Wilaya ya Nachingwea | 3,285 |
| | | Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa | 16,005 |
| | | Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa | 1,166 |
| 3 | Ruvuma | Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru | 31,212 |
| | | | |

# LIMETOLEWA NA
# BODI YA KOROSHO TANZANIA

S.L.P 533
Mtwara
Simu (Bure) : 0 800 112 159
Nukushi : (023) 2333536
Barua Pepe: info@cashew.go.tz

**MTWARA MAKAO MAKUU**

www.cashew.go.tz

**#Ajenda10/30**